Uhaba wa wahadhiri vyuoni unavyoitesa elimu ya juu
By Khalifa Said, Mwananchi ksaid@tz.nationmedia.com

Dar es Salaam. Hatua ya Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kufuta usajili wa baadhi ya vyuo vikuu ambayo mara nyingi huambatana na usitishaji wa udahili wa wanafunzi wapya, ni sawa na moshi tu katika moto unaoitesa elimu ya juu nchini.

Moja ya majukumu ya TCU ni kuhakiki ubora wa elimu inayotolewa na taasisi za elimu ya juu ili kubaini upungufu katika mfumo wake.

Miongoni mwa tatizo sugu katika sekta hiyo ni uhaba wa wahadhiri na wanataaluma wenye sifa, hususani wale wa ngazi ya uprofesa na shahada za uzamivu.

Kada hizo za wanataaluma ndizo hasa zinatakiwa kuwa nyenzo kuu za urithishaji wa taaluma kwa maelfu ya vijana wanaojiunga na taasisi za elimu ya juu kila mwaka.

Utafifi uliofanywa na Chama cha Wafanyakazi wa Elimu ya Juu (THTU), mwaka 2017 unaonyesha kuwa taasisi za elimu ya juu zinakabiliwa na upungufu wa watumishi wa aina zote wakiwemo wanataaluma na waendeshaji.

Kamati maalumu iliyoundwa na chama hicho ilitembelea baadhi ya taasisi na kutoa ripoti iliyoonyesha kwamba kwa sasa kuna upungufu wa asilimia 44 kwa watumishi wanataaluma pekee waliopo katika taasisi za umma.

Kamati pia ilibaini kuwa asilimia 53 ya watumishi wanataaluma katika ngazi ya uandamizi na kuendelea waliopo kwa sasa wamestaafu na hivyo wanafanya kazi kwa mikataba au wanatarajia kustaafu hivi karibuni na wataingia kwenye ajira za mikataba.

Pia inaonyesha kuna upungufu wa wastani wa asilimia 41 ya watumishi waendeshaji katika taasisi zilizotembelewa na kamati hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya THTU, upungufu huo ulionekana katika kada zote za watumishi waendeshaji.

Miongoni mwa vyuo ambavyo ripoti hii inavitaja kuwa na uhaba mkubwa wa watumishi wanataaluma ni Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya Muhimbili (Muhas) ambacho kina upungufu wa asilimia 65 na Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (Must) chenye upungufu wa asilimia 54.

Ripoti hiyo kiasi fulani inaungwa na ripoti ya uhakiki wa wafanyakazi wanataaluma iliyofanywa na TCU mwaka 2016.

Ripoti hiyo ilibainisha upungufu mkubwa katika kada mbalimbali za taaluma kwenye taasisi za elimu ya juu nchini.

Kwa upande wa afya ilibaini kuna upungufu wa wanataaluma 228 (asilimia 11.7), elimu 669 (asilimia 34.3), sayansi na teknolojia 897 (asilimia 45), uhandisi 59 (asilimia 3), sheria 14 (asilimia 0.7), biashara na uchumi 24 (asilimia 1.2) sanaa, sayansi ya jamii 60 (asilimia 3.0.)

Takwimu kutoka TCU zinaonyesha kuwa kuna jumla ya wahadhiri 3,448 wanaofundisha katika taasisi za elimu ya juu nchini.

Kati ya hawa, 274 ni maprofesa, 376 ni maprofesa wasaidizi, 783 ni wahadhiri waandamizi na 2015 ni wahadhiri wa kawaida.

Kwa mujibu wa TCU, hadi Februari 2016, Tanzania ilikuwa na vyuo vikuu vinavyojitegemea 30, vyuo 16 na kampasi, vituo na taasisi 22 za elimu ya juu.

Sababu za upungufu zatajwa

Mazungumzo ambayo Mwananchi imefanya na wadau wa elimu ya juu yanataja sababu za upungufu.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyakazi Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Udasa), Dk George Kahangwa anaamini kuwa kasi ya ongezeko la idadi ya vyuo vikuu vinavyojipanua kila kukicha kwa kuanzisha kampasi maeneo mbalimbali nchini inachangia ukubwa wa tatizo la upungufu wa wanataaluma.

Kasi hiyo haijaendana na uzalishaji wa wanataaluma wa kutosha ambao wangeweza kufundisha katika vyuo hivyo.

Anasema, “Wanataaluma waliokuwepo (miaka ya 1990) punde wakastaafu na hii ikasababisha usumbufu mkubwa kitu ambacho kimesababisha wengi wao kubakizwa na kuombwa kutostaafu.”

Dk Kahangwa anasema katika miaka ya 1990 Serikali ilizuia kuajiri wanataaluma wapya - zuio lililodumu kwa kipindi cha miaka kumi na hivyo kuzaa matatizo mengine mapya yanayoendelea kuisumbua elimu ya juu hadi sasa.

Hata hivyo, anaona pia kuwa Serikali inaviona vyuo vikuu kama eneo la ‘kuchota’ wataalamu wake.

“Ni ukweli usiofichika kwamba tangu aingie madarakani Rais Magufuli ameonyesha kuvutiwa na maprofesa na wale wenye shahada za uzamivu kutoka vyuo vikuu mbalimbali huku akiwateua kuwa mawaziri, manaibu waziri, makatibu wakuu na wakuu wa mashirika kadhaa ya umma,” anasema.

Moja kati ya vyuo vinavyotajwa kuathirika kwa kiasi kikubwa na hatua hii ni UDSM ambacho mpaka sasa, kwa mujibu wa Dk Kahangwa zaidi ya wanataaluma 30 wameshachukulia na Serikali.

Lakini Profesa Boniventure Rutinwa ambaye ni naibu makamu mkuu wa UDSM upande wa taaluma anasema hakuna tatizo kwa chuo kuchangia wanataaluma kwenda serikalini. “Ni wajibu wetu (kama chuo),” anasema. “Na hiyo idadi inaonekana kubwa kwa sababu hao wanaoteuliwa wanachukua nafasi kubwa tu za utumishi zinazoonekana na wengi.”

Profesa Rutinwa anahoji, “Inawezekanaje wanataaluma 30 wakaonekana wengi kati ya 1,300 wanaopatikana hapa chuoni?”

Tatizo la upungufu wa wahadhiri katika taasisi za elimu ya juu nchini linasababishwa pia na uhaba wa wasomi wa hadhi ya uprofesa na shahada za uzamivu katika soko la ajira.

Mwenyekiti THTU, Dk Paul Luisulie anasema hilo limekuwa ni tatizo sugu kwani hata kama vyuo vingetaka kuajiri wahadhiri upatikanaji wao ni mgumu.

Anasema hata wakipatikana wachache sana ndio hukidhi vigezo vya kuwa wahadhiri (na si kila profesa na mwenye shahada ya uzamivu anaweza kuwa mhadhiri.)

Hili linathibitishwa na Profesa Rutinwa ambaye anakiri UDSM kupokea kibali cha kuajiri wahadhiri wapya kutoka serikalini, lakini wanashindwa kuwapata wa kiwango kinachotakiwa.

Anasema, wachache wanaopatikana na kuwa na vigezo hupendelea kufanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali kwani huko wanalipwa zaidi kuliko kufundisha vyuoni

Pia, lipo suala la gharama ya kuendeleza wahadhiri na kufikia hadhi ya uprofesa au shahada ya uzamivu.

Hii ndiyo sababu inayomfanya Dk Aikande Kwayu, Mtanzania anayefundisha Chuo Kikuu cha Wisconsin, Marekani, kusema kuwa uhaba wa wahadhiri ni suala la kimfumo ambalo linahitaji uwekezaji mkubwa wa rasilimali kuweza kulitatua.

Hata hivyo, Dk Kahangwa kwa upande wake anaonya kwamba kama hali itaachwa iendelee kama ilivyo sasa hakuna atakayeweza kuzuia ubora wa elimu ya juu kuporomoka.

Msomi huyo anasema moja ya hatua zinazoweza kusaidia kupunguza tatizo hilo ni kurejeshwa kwa utaratibu wa kuwabakiza wanafunzi hodari wanaohitimu vyuoni na kuendelezwa mpaka kuwa wahadhiri kamili.

Naye Dk Kwayu anasema kuna haja ya kuliunganisha suala la uendelezaji wa wahadhiri vyuoni na mipango ya maendeleo ya Taifa kama vile Dira ya Taifa ya 2025 na ajenda ya viwanda. “Hatuwezi kuwa na kiwanda cha nguo, kwa mfano, kama hatuna wanataaluma watakaofanya tafiti katika eneo hilo,” anasema.

Hata hivyo *Dk Luisulie anaishauri Serikali kuanzisha utaratibu wa kuvikopesha vyuo ili kuendeleza wanataaluma wake kusaidia kupunguza tatizo lililopo hivi sasa.*